

MAJILIO 2026 – WIKI YA 5

AMEFUNGWA!

Mwokozi Aliyekuja katika Udhaifu kwa Ulimwengu Unaomngojea

Lucas 2:1–14



**“Watu wale
waliokwenda katika giza
Wameona nuru kuu;”**

Isaya 9:2 (SRUV)



Usiku huu tunawasha mshumaa wa KRISTO.

**Kusubiri kumekwisha. Ahadi imetimia.
Nuru imekuja, si kwa ajili yetu tu, bali kwa ajili ya kila
taifa, kila jamii na kila moyo.**



**Yesu alikuja akiwa amefungwa kwa nguo
za kitoto, akiwa amevikwa ubinadamu
na amezungukwa na upendo.**

**Aliingia katika ulimwengu wetu akiwa katika hali ya
udhaifu na unyenyekevu, akileta habari njema za furaha
kuu kwa watu wa mataifa yote.**



**Tumdhihirishe Mwokozi katika
maisha yetu na kuishiriki nuru
yake na ulimwengu.**

Kristo aliyekuja kwa ajili ya watu wa mataifa yote
adhihirishwe kupitia kwetu.



**Nuru ya ulimwengu, tunakushukuru
kwa kuja katika giza letu ukiwa na
upendo wako unaong'aa.**

Nuru yako iangaze katika kila utamaduni, kila lugha na kila taifa. Liwezeshe
Kanisa lako kuipeleka nuru yako kwa ujasiri na furaha. Mshumaa huu
utukumbushe kwamba habari ya Krismasi ni kwa ajili ya ulimwengu mzima,
na kwamba sisi ni sehemu ya utume wako wa kuishiriki.

Amina.

